Mwongozo wa Ushirikishaji Jamii na Miradi ya Ubia (PPP) kwa Halmashauri:

---

Rasimu ya Mwongozo wa Ushirikishaji Jamii na Miradi ya Ubia (PPP) kwa Halmashauri unawekwa wazi kwa umma ili kuweza kupata michango na mapendekezo ya wadau.

Mwongozo huu umeandaliwa na Kitengo cha Miradi ya Ubia, Ofisi ya Rais – Tawala za MIkoa na Serikali za Mitaa (PPP Node, PO – RALG), chenye wajibu wa kuratibu Mpango wa Miradi ya Ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP) ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mwongozo unatoa mtiririko wa kiutendaji wa jinsi ya kuishirikisha jamii katika Miradi ya Ubia wa Serikali na Sekta Binafsi (PPP). Mwongozo unajumuisha nadharia ya mrejesho kwa pande zote mbili; pamoja na umuhimu wa kusikiliza na kupokea michango ya jamii katika miradi hii ya ubia, lakini muhimu pia kutoa taarifa na kuitaarifu jamii kuhusu mradi husika.

Lengo kuu ni kuboresha na kufanikisha utekelezaji wa miradi ya ubia kwa kukusanya na kuyafanyia kazi mawazo na maoni ya jamii kuhusu mradi.

Tunashukuru sana endapo tutapata mawazo na maoni (mrejesho) kuhusu mwongozo huu hadi Septemba tarehe 30 2019.

Wakati maoni yote yatapokelewa na kufanyiwa upembuzi, hailazimu maoni na mapendekezo hayo kuingizwa moja kwa moja kwenye mwongozo. Hata hivyo, baada ya zoezi la ukusanyaji maoni/michango politachapishwa jedwali la kina, likiorodhesha michango, maoni na mapendekezo pasipo kutaja mtu, shirika au taasisi itakayowasilisha maoni.

**Shirika la Benki ya Dunia** (World Bank) linasaidia Wizara ya TAMISEMI kupitia ***Mpango wa Uendelezaji wa Miradi ya Ubia – Tanzania***, unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID). Mpango huu umeanza utekelezaji wake tangu mwaka 2017 kuzisaidia Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Serikali Kuu na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuandaa miradi ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi nchini. Hadi sasa kuna takribani miradi 50 ya ubia inayopokea msaada kupitia mpango huu.

**Tunatanguliza Shukrani za dhati kwa kuwasilisha maoni na mawazo yako!**